

KULE KUTOKA KWA TATU

Ufunuo 18:4, “ *Kisha nikasikia sauti nyingine kutoka mbinguni, ikisema, Tokeni kwake enyi watu wangu, msishiriki dhambi zake, wala msipokee mapigo yake*”

sikiliza kile Nabii wa Mungu amesema kuhusu hilo

²⁸⁵ Mungu alichagua katika siku za kutoka, Yeye alitoa nje kundi na kutoka kwenye lile kundi... Nataka muone jambo Fulani. Yeye alikuwa na wawili pekee, wale waliokwenda kwenye Nchi ya Ahadi (Hesabu 32:6-12; Joshua 14:6-15). Yeye alichagua nini cha kuwatoa nje? Siasa? Shirika la dini?. Alichagua nabii mwenye ishara ya kiungu ya nguzo ya moto kwamba watu wasingelikosea (kutoka 3:-10). Kile yule nabii alichosema kilikuwa ukweli. Mungu alishuka chini kutoka nguzo ya moto na kujidhihirisha mwenyewe, alionyesha Neno lake. Hilo ni sahihi?

²⁸⁶ Hicho ndicho Yeye alileta katika kutoka kwake kwa kwanza. Kutoka kwa pili... Yeye ni mkamilifu katika tatu. Ninyi nyote mnaona kuhubiri kwangu, siku zote ni tatu na saba. Saba ni kumaliza; tatu ni ukamilifu wake. Mvuto wa kwanza, wa pili na wa tatu na o-o-oh na kuendelea na kuendelea – kila kitu, unaona kuhesabiwa haki, utakaso, Ubatizo wa Roho Mtakatifu, Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, kila kitu. Unaona?

²⁸⁷ Angalia, yeye alifanya nini, kule kutoka kwa kwanza? Yeye alituma nabii, mwenye upako wa Nguzo ya moto, Naye aliwaita watu nje. Hivyo ilikuwa kutoka kwake kwa kwanza. Na ule wakati wa Israeli ulikuwa umefika, alituma tena Nabii – Mungu akiwa na nguzo ya Moto. Yohana aliiona ikishuka kutoka mbinguni kama hua (Yohana 1:29-34; Yohana 16:28). Na yeye akasema, “ Nakwenda kwa Mungu, na narudi kwa Mungu.”

²⁸⁸ Baada ya kufa kwake, kuzikwa, na kufufuka, Sauli wa Taso, akiwa njiani mwake kwenda Dameski, aliona ile ile Nguzo ya Moto. Na yeye akiwa Mwebrania, aliyefundishwa vyema katika Neno, akasema, “Bwana Wewe ni Nani?” Yeye alijua ile nguzo ya moto ilikuwa Bwana, yeye ni mwebrania. Akasema wewe ni nani? (matendo 9:1-8). Nayeye akasema mimi ni Yesu

²⁸⁹ Na hapa Yeye aliahidi jambo lile lile lililokuwa katika kutoka kutokea katika siku za mwisho, na Yeye hawezi kulibadilisha (Malaki 4:5-6).

Kwa uthibitisho wa kisasanyansi, kwa ushahidi wa Roho, kwa matendo ya yule Roho tunalionga hilo leo, ile nguzo kuu ya moto ikitembea miongoni mwetu. Na zile ishara na maajabu na ufufuo wa Yesu Kristo ukiita watu kutoka kwenye udhehebu nakuvingia katika uwepo wa Yesu Kristo kuishi; kwenda kwenye nchi.

²⁹⁰ Hakuna kosa, marafiki; siyo kile ninachosema; mimi ni ndugu yenu tu; lakini ni kile Mungu anachothibitisha kwenu. Hilo linakifanya kiwe ile kweli, ile ile nguzo ya moto Yeye

aliyoitumia katika nyakati zile mbili, Yeye ameileta miongoni mwenu leo na kuihakikisha hiyo Kisayansi.

²⁹¹ Kama mjuavyo, gazeti la life liliweka katika toleo lao la mwezi uliopita, pale wingu la maili ishirini na sita kwenda juu katika sura ya piramidi: Malaika saba waliwakilishwa ndani pale na wakaleta...na walikuletea wewe Neno la Mungu, chini ya uvuvio, na linawaambia ninyi juu ya saa hizi mnazozijia na kuishi ndani yake. Akili za kiroho zitachukua hilo sasa hivi na kulidaka. Ni kutoka! Tunakwenda kuondoka, mojawapo ya siku hizi. Mungu na ashukuriwe.

Sasa siri zote za kuhesabiwa haki kwa Imani, kutakaswa, na ubatizo wa Roho Mtakatifu vimeshaelezwa. Sasa, nikuchukua vipengele visivyokamilishwa ambavyo vimefungiwa katika Mihuri 7, siyo nyakati saba za kanisa, ile mihuri saba imefunua siri,

²⁹² Tazama, ile Nguzo ya Moto ile iliyowaita wale nje, iliwaongoza kwenda nchi ya ahadi chini ya upako wa nabii. Nguzo ya Moto ambayo waliitazama, iliwaongoza kwenda katika nchi ya ahadi chini ya nabii aliyepekwa mafuta (Musa). Na mara kwa mara walimkataa. Hilo ni sahihi? Hakika.

Litazame hilo tuko katika kuitwa nje “Tokeni Babeli, watu wangu,” ikasema sauti ya Malaika (Ufunuo 18:4-5). Nje ya nini? machafuko.

²⁹⁶ Je Methodisti liko sahihi? Au Babtisti? Au Katoliki? Tokeni kwake! Mungu yuko sahihi. Unajuaje? “Hebu kila neno la mwanadamu liwe la uongo na langu ukweli.” Tokeni kwake. Unajua kitu gani? Ile ile Nguzo ya moto, Roho yule yule wa atiaye mafuta, akiongoza kwenda nchi ya ahadi. Tazama, aliwaongoza, aliwatoa nje, akawaongoza kwenda nchi ya ahadi, Israeli, lile Taifa; na Mungu yule yule, nguzo ya moto ile ile.

³⁰¹ Kama wewe umechaguliwa; ile mbegu inaanguka juu ya udongo mkavu au juu ya miamba, kamwe haitafanya chochote. Migumu, mioyo ya jiwe inayotaka kuwa na kutojali, lakini kama ikianguka juu ya ardhi nzuri iliyo laini ya imani, itazaa Mkristo, akizaa matunda ya Roho (Matayo 13:1-8; 18-23).

³⁰² Tazama, jinsi yule Mungu alivyofanya hilo. Sasa, Yeye anayo ile ile Nguzo ya Moto; ile iliyothibitishwa. Mtu fulani alisema, “kwa nini usiende kuwaambia wale wanasayansi kuhusu hilo?” Unadhani wataliamini hilo? “usitupe lulu zako mbele ya nguruwe.” Yesu alisema tusifanye hivyo; sina uongozi wa kufanya hilo. Bado nikiwa ninaishi hapa hapa katika mji, pale walipokuwa wakitafuta kujua hilo. Nilifikiri ni ngekwenda kule chini, Roho mtakatifu akasema kaa mbali sio kwa ajili yao. Rudi na ukaliambia Kanisa.”

³⁰³ Vema na itatukia... kama kile wanachosema kitatukia, basi kumbuka, mimi nimenena,” Bwana alisema, unaona, kabla halijatukia, linatukia pale. Sikiliza Biblia. Ni sauti ya Mungu ikikuita katika siku hii.

²⁹⁹ sasa, nataka muone, hii hii nguzo ya moto inaongoza watu tena kwenda nchi ya ahadi, ule utawala wa Miaka Elf, pale tulipokuta chini ya uvuvio wa huu muhuri wa sita, hilo ambalo halikuwahi kamwe kufundishwa kabla, jinsi dunia inabidi itakaswe kwa ajili ya ule utawala wa miaka Elf. Ile Nguzo ya moto inawaongoza kwenda kwenye utawala wa miaka Elf. (Isaya 65:17-25). [1]

Roho Mtakatifu akiwa katika umbo la nguzo ya moto. Mungu akija chini katika udhihirisho ulioleta kule kutoka kwa kwanza na kuwatoa Israeli watoke Misri. Kule kutoka kwa pili ilikuwa Kristo akilitoa kanisa kutoka kwenye dini ya Kiyahudi. Na kutoka kwa tatu ni wakati nguzo ya moto inamchukua Bibi Arusi kutoka kwenye Kanisa unaona? Kutoka kile

kitu cha kiasili, kutoka kile cha kiroho, na cha Kiroho kutoka kwa cha kiroho hizo tatu. Unaona? Kile cha kiroho kutoka kanisani, tuseme hivyo na sasa tunapata zile Nyakati tatu za hilo [2].

Mtazame yule malaika wa Bwana katika nguzo ya moto. Uchunguzi wa kisayansi ukaipeleka ulimwenguni, wakijua kuwa wanakwenda kuhukumiwa nayo. Yule malaika wa Bwana ambaye alikuwa Kristo...

317 Ile nguzo ya moto iliwaongoza kwenda wapi? Sasa, kumbuka, Musa hakuwa ile nguzo ya moto. Yeye alikuwa kiongozi aliyepakwa mafuta chini ya ile nguzo ya moto. Na nguzo ya moto ilithibitisha tu ujumbe wake, kwa ishara na maajabu. Na ile nguzo ya moto iliwaongoza kwenda nchi ile Mungu aliyo waahidia wao, pale Yeye, Yeye Mwenyewe, Angefanyika mwili miongoni mwao siku fulani. (Yohana 1:1-3, 14-16). Hilo ni sahihi? Walifanya nini? Walinung'unika/kuwa na uchungu na kila kitu kingine, kuonyesha ilikuwa chini ya damu ya mwana kondoo wa kawaida.

318 Lakini, wakati huu –Utukufu kwa Mungu!-ile nguzo ya moto ile tunayoiona miongoni mwetu, ile nguzo ya moto itatuongoza kwenye utawala wa Miaka Elfu, pale Yeye atakaporudi kwa watu wake katika ule wakati wa kumiliki wa utawala mkuu wa miaka elfu baada ya huku kutoka, pale ambapo tutaishi umilele pamoja naye (Zakaria 14:16-21) Siku zote Yeye ana lile Neno la Baba, siku zote huthibitisha kuwa hilo ni sahihi.

319 Tuko katika kutoka, ee marafiki zangu, ndugu zangu, nyote mliopo hapa na wale watakaosikia kanda hebu mimi kama ndugu yenu na raia wa ule ufalme wa Mungu, Tokeni nje, katika huku kutoka!

320 kwani wote wale wanaobaki nyuma watapata Alama ya Mnyama. Tokeni Babeli; tokeni katika haya machafuko; tokeni katika hii mipango na mumtumikie Mungu. Aliye hai. Hebu huyo Malaika mkuu wa Agano, Yesu Kristo katika hili umbo la Mungu, hakuwaza kule kuwa sawa na Mungu ni kitu cha kushikamana nacho (Filipi 2:5-10). Sasa, Yeye ni nguzo ya moto katika lile lile umbo ambalo Yeye alikuwa nyuma kule akileta kule kutoka kwa kwanza, akileta kutoka kwa pili, na hapa akiwa na kutoka kwa tatu.

321 Kutoka kwa kwanza, yeye alifanya nini? Aliwaleta nje toka nchi ya asili kwenda nchi ya asili. Kutoka kwa pili, Yeye aliwaleta nje toka hali ya kiroho kuingia ubatizo wa kiroho wa Roho Mtakatifu. Sasa yeye anawaleta toka ubatizo wa kiroho wa Roho Mtakatifu, kurudi moja kwa moja kuingia Nchi ya Milele ya utawala wa Miaka Elfu. Na mambo makuu baada ya hapa. Nguzo ile ile ya moto, kwa mfumo ule ule wa upako, Mungu yule yule akitenda mambo yale yale. Na neno lile lile lililomtangaza yule wa kwanza, lilimtangaza yule wa pili. Lile lile Neno lililomtangaza yule wa pili limemtangaza yule wa tatu, na hapa tunalionga miongoni mwetu.

322 Tokeni! Ee, tokeni nje ya haya machafuko! Njooi kwa Mungu Aliye hai. Njooi kwenye Neno! “Naye alifanyika mwili akakaa kwetu.” Na sasa, Yeye yupo ndani ya miili yetu, akikaa miongoni mwetu. Tokeni nje na mumtumikie Mungu aliye hai, (1Thesalonike 1:9-10) [1].

Na sasa, katikati ya siku, wakati kuna uzushi mwingi na mambo, hata hivyo, Mungu hujitambulisha mwenyewe. Sasa, tunaona hili, na jinsi lilivyo, la utukufu ni kujua hili, kwamba maskani yetu hii ya udongo, siku moja, mwili huu mzee, unaovunjika, kwamba tunaugua na kuteseka ndani yake, utabadilishwa na kufanywa kama ule wa kwake mwenyewe mwili wa utukufu (wafilipi 3:20-21). Ndipo tutakapomuona kama alivyo na kuwa pamoja katika nchi ambayo leo tumefungwa kwa hiyo (1Yohana 3:1-3). Ooh mimi

inanifanya nijisike kusimama na kuimba nimefungwa kwa nchi ya ahadi (“ukingoni mwa Yordani”) [3].

Nukuu:

[1] kutoka kwa tatu uk. 38-43,

[2] Je maisha yako yanaistahili Injili

[3] Lileshitaka.

Jiwe la kiroho la kujengea na 146 kutoka Neno lililofunuliwa la saa hii, iliyokusanywa na Gerd Rodewald, Friedenstr. 69, D- 75328 Schomberg Germany, simu (+49) 72357613 Fax (49) 72353306

Anakuja mmoja na ujumbe ambao utakuwa moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itaizunguka dunia. Zile mbegu zitaingizwa katika magazeti na vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu ya Mungu iliyoteuliwa kimbele imesikia hilo (ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724).

Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:

Charles E. Y. Kanju,

Box 553 Korogwe - Tanga

E-mail: Chaelika@livel.com

Cellphone: 0784 704299/ 0718230098